

**MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOFANYIKA KATIKA  
UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA TAREHE 29/10/2021**

**WATAALAM WALIOHUDHURIA**

- |                             |                                                 |
|-----------------------------|-------------------------------------------------|
| 1 Ndg. Butamo Ndalaha       | - Mkurugenzi Mtendaji(W) - Mwenyekiti           |
| 2 Ndg. Ruth N. Mwelo        | - Afisa Utumishi na Utawala (H/W) - Katibu      |
| 3 Ndg. Prediganda Valerian  | - TSC                                           |
| 4 Ndg. Evelyn Ngwira        | - Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (H/W)   |
| 5 Ndg. Evans Mwalukasa      | - Kaimu Mweka Hazina (H/W)                      |
| 6 Ndg. Brown H. Nziku       | - Afisa Ardhi na Maliasili (H/W)                |
| 7 Ndg. Peter N. Mboje       | - Kny: Afisa Manunuzi na Ugavi (H/W)            |
| 8 Ndg. Frank Mkude          | - Kaimu: Mkuu wa Idara ya Ujenzi (H/W)          |
| 9 Ndg. Sijaona Muhunzi      | - Mratibu wa Mfuko wa Kijiji(H/W)               |
| 10 Ndg. Peter Mundo         | - Kny: Mwanasheria (H/W)                        |
| 12 Ndg. Doris Hugo          | - Mkaguzi wa ndani                              |
| 13 Ndg. Festo Lyimo         | - Kny: Mganga Mkuu (H/W)                        |
| 14 Ndg. Shaban Ruseya       | - Afisa Biashara (H/W)                          |
| 15 Ndg. Christina Samwel    | - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki (H/W) |
| 16 Ndg. Victoria Mtengie    | - Mratibu wa UKIMWI                             |
| 17 Ndg. Joseph Biruma       | - Kny: Afisa Elimu Msingi (H/W)                 |
| 18 Ndg. Mwanila Sembina     | - Kaimu A/Mtendaji M/M/Mlandizi                 |
| 19 Ndg. Nicodemus Mombia    | - Afisa Wanyamapori                             |
| 20 Ndg. Ombeni Msangi       | - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)                     |
| 21 Ndg. Doris Semkiwa       | - Kny: Afisa Elimu Sekondari (H/W)              |
| 22 Ndg. Beatha Kassian      | - Kny: Afisa Mipango (H/W)                      |
| 23 Ndg. Mahamodu Mrutu      | - Kny: Afisa TEHAMA                             |
| 24 Ndg. Maximilian E. Mtobu | - Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (H/W)          |

**SEKRETARIETI**

- 1 Ndg. Mariam Lambileki
- 2 Ndg. Adam Masinde

**KDC.CMT.NA.01/10/01/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na aliwataka kuwa wasikivu na wepesi wa kuchangia mada, hatimaye alifungua kikao saa 06:02 mchana.

**KDC.CMT.NA.01/10/02/2021: KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 29/10/2021**

Wajumbe walizipitia agenda sita (06) zilizowasilishwa na Katibu. Wajumbe kwa kauli moja waliridhia ziwe agenda halali za kikao hicho.

**KDC.CMT.NA.01/10/03/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA MENEJIMENTI 12/09/2021**

Wajumbe waliupitia muhtasari ukurasa kwa ukurasa bila kufanya marekebisho yoyote, wajumbe waliridhia muhtasari huo uthibitishwe na usainiwe ili uwe kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**KDC.CMT.NA.01/10/04/2021: MAPOKEZI YA FEDHA TSH.850,000,000.00 KWA AJILI YA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19**

Afisa Mipango(W) aliwasilisha taarifa kuwa, Katika Mapambano Dhidi ya UVIKO – 19, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada zake za kupambana na UVIKO - 19 amewezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kupata mkopo wenye masharti nafuu kiasi cha **Shilingi trillioni 1.3** kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO -19 ili kuchangia, kufufua uchumi kwa Sekta zilizopata athari za kiuchumi kutokana na madhara ya ugonjwa huo. Matumizi ya Fedha hizi zimeelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vinavyogusa wananchi moja kwa moja kwa ajili ya kuwaondolea kero katika kuzifikia na kupata huduma za afya, elimu na kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanya biashara wadogo/vajasiriamali wakiwemo wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Katika fedha hizo Halamashauri imeidhinishwa jumla ya **Tshs. 850,000,000.00** kwa utekelezaji wa Miradi ya Elimu na Afya kwa mchanganuo ufuatao:-

- (i) Vyumba vya Madarasa 20 ya Shule za Sekondari kwa gharama ya Shilingi 400,000,000.00.
- (ii) Vyumba vya Madarasa 10 vya shule shikizi za Msingi yatajengwa kwa gharama ya Shilingi 200,000,000.00.
- (iii) Ujenzi wa Mabweni mawili (2) Shule za Msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji Maalum kwa gharama ya Shilingi 160,000,000.00.
- (iv) Ujenzi wa Nyumba 1 ya watumishi wa Afya yenye uwezo wa kuchukua familia tatu (3) ambazo zitagharimu kiasi cha Shilingi 90,000,000.00.

Hadi kufikia tarehe 28/10/2021 Halamashauri imepokea jumla ya **Tshs. 600,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa. Kati ya fedha hizo **Tshs.400,000,000.00** ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 20 vya madarasa katika shule za Sekondari ikiwa ni maandalizi ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022. **Tshs.200,000,000.00** ni kwa ajili ya madarasa 10 ya shule shikizi za Msingi.

Mchanganuo wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Idara ya Elimu Sekondari umetokana na mahitaji ya shule kwaajili ya mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2022. Jedwali linaonesha mchanganuo wa ujenzi wa vyumba hivyo.

| NA | KATA         | JINA LA SHULE   | IDADI YA VYUMBA VYA MADARASA | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA |
|----|--------------|-----------------|------------------------------|-------------------------------|
| 1  | KILANGALANGA | DISUNYARA       | 4                            | 80,000,000.00                 |
| 2  | KILANGALANGA | KILANGALANGA    | 2                            | 40,000,000.00                 |
| 3  | MLANDIZI     | DOSSA AZIZ      | 2                            | 40,000,000.00                 |
| 4  | MLANDIZI     | MIHANDE         | 2                            | 40,000,000.00                 |
| 5  | SOGA         | RAFSANJANI SOGA | 4                            | 80,000,000.00                 |
| 6  | KWALA        | KWALA           | 1                            | 20,000,000.00                 |
| 7  | MAGINDU      | MAGINDU         | 2                            | 40,000,000.00                 |
| 8  | KAWAWA       | KAWAWA          | 3                            | 60,000,000.00                 |
|    |              | <b>JUMLA</b>    | <b>20</b>                    | <b>400,000,000.00</b>         |

Idara ya Elimu Msingi imeingiziwa fedha kwaajili ya ujenzi wa shule shikizi kwa mchanganuo ufuatao.

| NA | KATA   | SHULE    | KITUO SHIKIZI | IDADI YA MADARASA | KIASI CHA FEDHA KILICHOINGIZWA |
|----|--------|----------|---------------|-------------------|--------------------------------|
| 1  | DUTUMI | DUTUMI   | MWEMBENGOZI   | 5                 | 100,000,000.00                 |
| 2  | KAWAWA | MSONGOLA | MKOMBOZI      | 5                 | 100,000,000.00                 |
|    | JUMLA  |          |               |                   | 200,000,000.00                 |

Taarifa ilipokelewa na wajumbe walijadili yafuatayo:-

Mjumbe mmoja akichangia hoja alieleza kuwa, fedha hizo zimeletwa lengo likiwa ni kupeleka huduma muhimu kwa wananchi, wao kama Menejimenti wajipange kuhakikisha zinasimamiwa vizuri na kila mmoja anatimiza wajibu wake.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa ushauri wa mjumbe mtoa hoja ni mzuri, kinachotakiwa watu wa Idara ya Ujenzi, Idara ya Elimu Sekondari na Msingi na Kitengo cha Ununuzi na Ugavi kwa kushirikiana na Afisa Mipango (W) wahakikishe taratibu zote zinafuatwa ikiwa pamoja na kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha miradi yote inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa na ikamilike kwa wakati uliopangwa.

Wajumbe kwa pamoja baada ya majadiliano hayo waliridhia mapokezi ya fedha hizo na walikubaliana utekelezaji wake uanze mara moja.

#### **KDC.CMT.NA.01/10/05/2021: MAOMBI YA KUBADILISHA VIFUNGU (BUDGET REALLOCATION)**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri inaomba kutanua vifungu vyenye Jumla ya Tshs. 250,444,239.98 ambavyo hadi kufikia mwezi Disemba, 2021 haviwezi kutumika kutokana na vifungu hivyo kutokuwa na fedha.

Wajumbe walipokea taarifa na walishauri ipelekwe kwenye kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa ajili ya kuidhinishwa

#### **KDC.CMT.NA.01/10/06/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwashukuru wajumbe kwa ushauri waliutoa na aliagiza kila mtu atomize wajibu wake na washirikiane katika utekeleza wa miradi hiyo ya UVIKO- 19 ili iweze kukami kuyafanyia kazi mapema kama kikao kilivyoagiza. Kisha Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na alifunga kikao saa 09:05 Alasiri.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA:**

Butame N. NDALAHWA  
JINA LA MWENYEKITI

SAHIHI: [Signature]

TAREHE: 19/11/2021

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**KIBAHA**

RUTH N. MWERO  
JINA LA KATIBU

SAHIHI: [Signature]

TAREHE: 19-11-2021